# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**STRATHMORE HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# STRATHMORE SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**KARATASI YA 2**

**LUGHA**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**MAJIBU YA UFAHAMU**

(a) Upeo wa Kiswahili, Kiswahili, Historia ya Kiswahili n.k. (Mwalimu akadirie jibu) (1 x 2) Al. 2

(b) (i) Utafiti na uchambuzi hauna umakinifu
(ii) Mtazamo uliotumiwa unaegemea taaluma moja tu (2 x 1) Al. 2

(c) (i) Kutafiti jiografia pana na ndefu ya lugha ya Kiswahili
(ii) Kutazama uhusiano wa karibu wa kuishi pamoja
(iii) Kutazama u-nje wa lugha ulioko ndani ya historia ya lugha ya Kiswahili
(iv) Kuangalia mfumo wa maisha ya wazawa wa lugha na wasiokuwa wazawa.
(v) Kutazama na kutofautisha Nyanja mbalimbali za taaluma (Al. 5 x 1)

(d) Katika kupanua lugha kwa mtazamo na mahitaji ya lugha yenyewe katika lugha yenyewe (Al. 2)

(e) (i) Inasotasota – Polepole au kukweta
(ii) Umakinifu – Uzingatifu
(iii) Isimu Jami – Uhusiano wa lugha na Jamii
(iv) U-nje – Sifa za kawaida za lugha (Al. 4)

2. **UFUPISHO**

(a) (i) Dhana ya kupatilizwa inatokana na hofu ya vita
(ii) Sababu za vita hazikuzushwa na Sayansi
(iii) Sayansi imekuza ujuzi wa vita na kuupotoa
(iv) Imeziongeza nguvu za wachochezi wa vita
(v) Zana za kisasa zinaweza kufisha watu wengi
(vi) Hakuna taifa lililosita kuanza vita kwa hofu ya maangamizi
(vii) Uundwaji wa silaha hatari hautazuia vita (hoja 7)

(b) (i) Lawama ni kwa wataalamu wa Sayansi
(ii) Wamejiziba katika kunge za kupagaza waja na kujifanya waongo duniani
(iii) Kila mtu ataka awaepuke kwa hofu
(iv) Ni juu yao kuyaondosha maoni haya
(v) Tuifanye sayansi chombo cha kudumisha amani (hoja 5)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) (i) Wakati wa kutamka konsonanti sauti hubanwa ilhali katika kutamka irabu sauti haibanwi (1 x 2 = 2)
(ii) Sifa za sauti /0/
- Ni sauti ya kati
- Hutamkiwa nyuma ya ulimi
- Inapotamkwa midomo huwa imeviringwa (Zozote 2)

(b) Vivumishi
(i) Wa – Kivumishi cha 'a' – unganifu
(ii) Ile – Kivumishi kionyeshi (2 x1 = 2)

(c) Kutunga sentensi
Taka shufaa – Omba msamaha kwa kosa fulani
mf: Mirriam alimtaka shufaa rafiki yake kwa maudhi aliyomfanyia (1x1 = 1)

(d) Hali ya 'a'

Mwanafunzi hula wali – Mwanafunzi ala wali (1 x 1 = 1)

(e) Kukanusha

Asipofika mapema hatampata – Akifika mapema atampata (2 x 1 = 2)

(f) (i) Maana ya kihusishi – Ni neno linaloonyesha uhusiano baina ya neno na lingine au kati ya kundi la maneno na lingine (1 x 2 = 2)

(ii) Kuanisha vihusishi

Kutoka – Mahali

Hadi – Mahali (2 x 1 = 2)

(g) Kutunga sentensi

Mbali – tofauti

Bali – Kasoro (2 x 2 = 2)

Mwalimu akadirie jibu

(h)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| S √ ½ | | | | |
| KN √ ½ | KT √ ½ | | | |
| √ ½ | T √ ½ | N √ ½ | E √ ½ | S √ ½ |
| | Nilimwona | Mamba | Majini | Nilipopiga mbizi |

Alama ½ x 8 = 4

(i) Sifa za sauti /ng'/

-Ni king'ong'o

-Si ghuna (1 x 2 = 2)

(j) Sentensi ya rai

Mwalimu akadirie jibu

Mwanafunzi atumie maneno kama vile

Naomba, tafachali, nisaidie, nakusihi n.k

Asitumie Nipe

(k) Wingi

Kelele Za Wamchao Mungu ni Baraka

½ ½ ½ ½ (4 x ½) = 2)

(l) Kutunga kupitia muundo

mf: Alifika √ ½ mapema √ ½ sana √ ½ lakini mwalimu √ ½ wake √ ½ akamchapa √ ½ viboko √ ½ (alama 4)

(m) Tofauti kati ya kiwakilishi nafsi huru na nafsi ambata

Nafsi huru – Maneno kamili yanayotumika badala ya majina ya watu

Nafsi ambata – Viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya vitenzi ili kuwakilisha mtenda

(n) Usemi halisi

√ ½

" N aomba kitabu cha Kiswahili," Mwalimu alisema. ½ √ (6 x ½) (alama 3)

√ ½ √ ½ √ ½ √ ½

(o) Mofimu huru

Inayojisimamia kimaana mf: mtu, kalamu, bora nk. (1 x 1 = alama 1)

(p) Ukubwa – Wingi

Maguo yaliwekwa kando ya malango (2 x ½ = alama 1)

(q) Maana ya chagizo

Neno au maneno katika sentensi yanayotoa taarifa kuhusu kiarifa (kitenzi) al. 1

(r) Vishazi

Mg: mwanafunzi ataenda shuleni ingawa ana mafua

Mwanafunzi ataenda shuleni – kishazi huru
Ingawa ana mafua – Kishazi tegemezi )                2 x 1 = alama 2)

(s) Tanakali ya sauti tifu – kuanguka mchangani
Mwalimu akadirie jibu (1 x 1 = al. 1)

**4. ISIMU JAMII**

(a) Changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili

- Hakuna sera maalum kutoka kwa serikali
- Kuna uhaba Mwingi/mkubwa wa waandishi
- Kuzuka kwa lugha ya sheng' ambayo ni maarufu miongoni mwa vijana
- Imani potovu kuwa lugha ya Kiswahili ni duni
- Kuzuka kwa lugha zingine k.v Kifaransa, Kiingereza
- Watumizi wa Kiswahili hawajali jinsi ya kutumia lugha
- Ukosefu wa fedha za kufanya utafiti wa kina wa somo la Kiswahili

*(Zozote 5 x 1 al. 5)*

(b) Hatua za kuimarisha lugha ya Kiswahili

- Lugha ya Kiswahili imeteuliwa kuwa lugha ya taifa
- Hutumika katika matangazo na taarifa za habari kupitia runinga
- Viongozi wa dini wanahubiri wakitumia lugha ya Kiswahii
- Kenya na Tanzania zimeunda mabaraza ya vyama mbalimbali vya kushughulikia maenezi k.v CHAKITA na BAKITA
- Lugha hii imetumiwa na wanabiashara
- Lugha hii hufunzwa katika shule na vyuo
- Shughuli za sanaa, maonyesho na muziki
- Uchapishaji wa vitabu                *(Zozote 5 x 1 = alama 5)*